**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KATE

**MAY , 2026**

**RUKWA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI**

**Namba za Simu Mkuu wa Shule 0627345194**

**Makamu Mkuu wa Shule.0718552192**

**Matron/Patron 0621335455/0679719415**

**Shule ya Sekondari Kate**

**S.L.P. 194**

**Tarehe 06/05/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
.......................................................................
**S.L.P** .................................
..............................................

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KATE ILIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI MKOA RUKWA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii katika tahasusi ya HKL/HGL/HGL

Shule ya Sekondari Kate ipo umbali wa Kilometa 60 Kaskazini Magharibi mwa Mji wa SUMBAWANGA. Usafiri wa basi kutoka mjini SUMBAWANGA unapatikana katika kituo cha mabasi STENDI YA ZAMANI Nauli ni Shilingi 7000/= kwa na Shilingi 30,000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ......................

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Sketi nyeusi na kijani jeshi.kwa Wasichana na suruali nyeusi na kijani jeshi kwa Wavulana (ni vema kushonea shuleni kuepuka usumbufu na kukosea)





ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu;

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni NYEUPEifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni JEZI 2 NYEKUNDU Kwa wasichana na JEZI 2 NYEKUNDU pamoja na bukuta zake kwa wavulana , pamoja na viatu vya michezo.



v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi/khaki za shule;
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta Rangi ya bluu lenye shingo ya v
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni 2 za damu ya mzee kwa wasichana,kitambaa aina ya zari (kushona hapa ni vizuri kuepuka kukosea); wavulana truck suit 2 za kushindia.



x. Wasichana / wavulana waje na trucksuit nyekundu ya michezo pia
xi. Tisheti yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 makubwa aina ya quire 3
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa Geography.
v. Godoro kwa wanafunzi wa bweni la futi mbili na nusu. Aidha, godoro linaweza kupatikana shule kwa bei ya shilingi 65000/=(Godoro la Dodoma)
vi. Mashuka Jozi 2 ya bluu, blanket 1 jepesi, foronya ya godoro 1, chandarua 1

vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko rangi nyekundu.
x. Vifaa vifuatavyo
- Jembe kwa wanafunzi wa -HGL
- Reki kwa wanafunzi wa -HKL
- Mafagio na kwanja kwa wanafunzi wa -HGL1

## 2.3 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB; Gharama hizo hapo juu (80,000) zilipwe kwa account hii; KATE SCONDARY SCHOOL RECCURENT A/C NO. 62001100039 NMB na mwanafunzi aje na bank-pay-in-slip yenye jina lake.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule ; THOMAS L. MPANDASHALO**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ..** MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KATE

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0627345194**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0718552192**
- **Mwandamizi Taaluma 0629788127**
- **Mwandamizi Malezi 0620413510**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

***SHULE YA SEKONDARI KATE***

## FOMU YA KUTHIBITISHA AFYA.

**(Fomu hii inajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na kurudishwa kwa mkuu wa shule ya sekondari KATE**

*Jina la mwanafunzi.............................................................................*

*Tafadhari naomba kwamba uweze kumpima hali yake ya afya mwanafunzi mwenye jina hapo juu ili kumthibitisha kiasi chake cha afya kuweza kumdu shughuli za masomo darasani, kazi za mikono na michezo. Tafadhari weka alama ya ve (V) mbele ya eneo alilopimwa / kuchunguzwa kwenye neon HAPANA au NDIYO na iwapo ni NDIYO kwamba limeonekana tatizo basi eleza katika nafasi iliyowekwa.*

*J e, mwanafunzi ana tatizo lolote katika sehemu zifuatazo?*

1. *Uwezo wa kuona: MACHO* HAPANA..........NDIYO.......... ..........
2. *Uwezo wa kusikia* HAPANA.......... NDIYO.......... ..........
3. *Uwezo wa kusema: sauti* HAPANA.......... NDIYO.......... ..........
4. *Kifua kikuu TB* HAPANA.......... NDIYO.......... ..........
5. *Shinikizo la damu* HAPANA.......... NDIYO.......... ..........
6. *Ulemavu wa viungo* HAPANA.......... NDIYO.......... ..........
7. *Tatizo lolote la kiafya* HAPANA.......... NDIYO.......... ..........
8. *Akubaliwe kupokelewa kusoma* HAPANA..........NDIYO.......... ..........
9. *Kundi lake la damu ni ..............................................................................*
10. *Malalamiko mengine yoyote anayotoa mwanafunzi kuhusu afya au viungo vyake*

    ........................................................................................................................................................

11. *Kuna tatizo au ugonjwa kuhusiana na afya yake linaloweza kufanya mwanafunzi huyu alazimie kusoma shule iliyo karibu na hospitali ya wilaya au mkoa?*

    ........................................................................................................................................................

12. *Maoni na mapendekezo ya daktari apokelewe au asipokelewe kuendelea na masomo ya shule ya sekondari mwaka Huu:*

    ....................................................................................................................

........................ ........................ ....................

*J ina kamili la Mganga* *sahihi yako* *Cheo*

........................ ....................

*TAREHE* *MUHURI*

## FOMU YA KUKIRI KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.

**A:SEHEMU YA MWANAFUNZI**

MIMI ……………………………………………………………

Nikiwa mwanafunzi wa Shule hii nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndiyo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kulitumikia Taifa na kuletaMaendeleo.

Hivyo basi ninaahidi kwamba, nitajibidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ilikutimiza shabaha hiyo ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa na walimu wangu.

Nikiwa na malalamiko au maoni nitayafikisha kwa viongozi wa shule kufuatana na utaratibuuliowekwa bila ya kuongeza chochote. Nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili iwapo nitakuwa nimekiuka sheria za shule.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI ......................................TAREHE**

**B:SEHEMU YA MZAZI**

Mimi ...................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi mtajwa hapo juu,

naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule katika kumlea mwanangu. Hii ikiwa ni pamoja na kutomruhusu mwanagu kuja na simu shuleni. Nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba nitakuwa tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa iwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.

Sahihi ya mzazi/mlezi …………………………………………………………………………….

Namba ya simu ya mzazi/mlezi ……………………………………… Tarehe: ……………

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.